**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI *(PRESS RELEASE)***

**UFAFANUZI JUU YA HABARI ILIYOTOLEWA NA GAZETI LA JAMHURI LA TAREHE 15 – 21 APRILI, 2025 JUU YA WAKULIMA WA KOROSHO KUSAMBAZIWA VIUATILIFU VILIVYOKWISHA MUDA WA MATUMIZI**

Msimu wa mwaka 2024/2025 Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kwa niaba ya Serikali iliratibu usambazaji wa viuatilifu vya ruzuku vya zao la korosho ambavyo ni *sulphur* ya unga tani 41,263 na viuatilifu vya maji lita 2,689,581 kwa wakulima kwa ajili ya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa zao la korosho nchini. Kati ya viuatilifu hivyo lita 4,500 za Sky Plus 550EC vyenye viambata amilifu *(Active ingredients) profenofos 50g/l +cypermethrin 50g/l* vilisambazwa katika Mkoa wa Katavi kwa ajili ya kutumika mwaka 2024.

Hata hivyo, kupitia zoezi la tathmini ya usambazaji wa pembejeo kwa msimu wa mwaka 2024; CBT iliweza kubaini kiasi cha viuatilifu vya *sky plus* ambavyo vimeisha muda wake wa matumizi mwezi Machi, 2025 kubaki kinyume na matarajio kwamba wakulima wangevitumia msimu wa mwaka 2024. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kila mwaka viuatilifu vipya hununuliwa na kusambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kutumika katika msimu wa mwaka husika. Kufuatia hali hiyo wakulima walielekezwa kutovitumia wakati huku Bodi ikiendelea na utaratibu wa kuvikusanya viuatilifu hivyo ili kutoa fursa ya kusambazwa kwa viuatilifu vingine vipya ambavyo viko ndani ya muda wa matumizi kwa ajili ya msimu wa mwaka 2025. Zoezi la ukusanyaji wa viuatilifu hivyo tayari lilishaanza na linatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi Aprili, 2025 ili kutoa nafasi ya kusambaza viuatilifu vingine vya ruzuku kwa ajili ya msimu wa mwaka huu wa 2025. Hii ni kwa kuzingatia Kalenda ya Zao la Korosho kwamba sehemu kubwa ya wakulima wa Mkoa wa Katavi wanatarajia kuanza upuliziaji wa mikorosho kuanzia mwezi Mei, 2025.

Rai kwa wakulima wa korosho nchini, CBT inapenda kuwasihi na kuwasisitiza wakulima wote wa zao la korosho nchini kuhakikisha kuwa wapatapo mgawo wa viuatilifu kuhakikisha kuwa wanavitumia ndani ya msimu husika ili kuepuka kubaki navyo na hatimaye kufikia ukomo wa muda wake wa matumizi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kila mwaka Serikali hupanga bajeti ya kununua viuatilifu vipya kwa ajili ya kuwasambazia wakulima ili wavitumie ndani ya msimu wa mwaka husika. Serikali inawasambazia wakulima viuatilifu vyenye ruzuku ya 100% ikiwa ni miongoni mwa jitihada za kuwapunguzia gharama na kuwaongezea faida/kipato kutoka kwenye kilimo cha zao la korosho.




***Picha Na. 01:*** *Afisa wa Bodi ya Korosho Tanzania akiendelea na ukusanyaji wa Kiuatilifu aina ya Sky Plus 550EC ambacho kimeisha muda wake wa matumizi kutoka kwa wakulima wa korosho wa Mkoa wa Katavi.*

**Kuhusu Upatikanaji wa Soko la Uhakika**

Serikali inatambua changamoto ya masoko ya korosho ghafi hususani kutoka maeneo mapya yaliyoanza uzalishaji. Hii inatokana na uzalishaji mdogo kwa kuwa maeneo hayo ni mapya na kiwango cha uzalishaji bado kipo chini.  Katika kupata ufumbuzi wa changamoto hii; Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania imekuwa ikihakikisha kwamba inawatafutia masoko ikiwa ni pamoja na kuuza mazao hayo kupitia maeneo mengine yenye uzalishajj mkubwa ili kuongeza ushindani. Aidha, Bodi imeendelea kutoa elimu ya kuongeza thamani zao la korosho kwa wakulima na wabanguaji wa korosho ili kuongeza wigo wa kuuza korosho zilizobanguliwa pamoja na bidhaa zingine zitokanazo na korosho. Mathalani, katika msimu wa 2024/2025 na 2023/2024 baadhi ya wakulima wa mikoa mipya wamenufaika na bei nzuri ya korosho zao kutokana na kuhamasika kukusanya korosho ghafi kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani na kuziuza kwa pamoja na kuongeza thamani kwenye viwanda vidogo vilivyopo Katavi na Manyoni.

**Changamoto ya Huduma za Ugani**

Maeneo mapya yanayolima korosho yamekuwa na changamoto ya wakulima kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya kanuni za kilimo bora cha korosho. Katika jitihada za kutatua changamoto hiyo Bodi ya Korosho imeanzisha Tawi Mkoani Katavi ili kusogeza huduma za usimamizi karibu na wakulima. Aidha, Bodi inao wataalamu wa kilimo ambao wamekuwa wakishirikiana na maafisa kilimo wa Halmashauri husika. Bodi itaendelea kuimarisha huduma ya utoaji wa elimu kwa wakulima wa korosho Mkoani Katavi ili wakulima waweze kunufaika na zao hilo ipasavyo.

Imetolewa na:-

MKURUGENZI MKUU
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
TAREHE 15 APRILI, 2025